

HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE



TANGAZO LA ZABUNI LA MARUDIO

Kwa ajili ya Kutafuta mzabuni wa kukusanya taka ngumu na kutoza ushuru wa taka ngumu katika mji wa Inyonga (Eneo la Inyonga).

1. Halmashauri ya Wilaya ya Mlele imepanga kukusanya taka ngumu kwa mujibu wa sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004 kifungu cha 114 ambacho kinaeleza wajibu wa mamlaka ya serikali za mitaa kusimamia na kupunguza taka ngumu.
2. Halmashauri ya Wilaya ya Mlele inawaalika watu binafsi, kikundi au kampuni kuomba zabuni ya uzoaji wa taka na utozaji wa ushuru wa taka katika eneo la Inyonga kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.
3. Zabuni hii itafanyika kwa mujibu wa kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013, tangazo la serikali namba 446 na marekebisho yake ya kanuni za mwaka 2016.
4. Waombaji wa zabuni wanaweza kupata maelezo zaidi na kukagua nyaraka ya zabuni kutoka kwa katibu wa bodi ya zabuni toka Halmashauri ya Wilaya ya Mlele S.L.P 686 Mpanda, wakati wa masaa ya kazi kuanzia 2.00 asubuhi hadi saa 9.30 mchana kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu au mapumziko.
5. Waombaji wote wanatakiwa kulipia ada ya maombi kiasi cha T.shs 20,000/ (elfu ishirini tu) ambayo haitarejeshwa, malipo hayo yatafanywa kupitia akaunti ya Halmashauri, **Na 61910002713, MLELE DC OWNSOURCE COLLECTION ACCOUNT**, baada ya kupatiwa (Bill/Ankara/ Control number) toka ofisi ya Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.
6. Nyaraka za Zabuni za Kazi hii zinapatikana ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Kitengo cha Ugavi/Manunuzi kuanzia saa 2.00 (saa mbili

kamili asubuhi) hadi saa 9.30 (saa tisa na nusu alasiri), kuanzia tarehe 20.10.2021 hadi tarehe 27.10.2021 na kufungwa tarehe 27.10.2021 saa 4.00 (saa nne kamili asubuhi).

7. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 27/10/2021 saa 4.30 asubuhi na zabuni zitafunguliwa saa 5.00 asubuhi kwenye ofisi za manunuzi
8. Mzabuni atalipwa asilimia 70% na Halmashauri itabakia na asilimia 30% ya Mapato kutokana na Tozo ya Taka.
9. Maombi ya zabuni yanatakiwa kutumwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na kuonesha aina ya zabuni inayoombwa bila ya kuwa na alama yoyote ya kuashiria ilikotoka na itumwe kwa anuani ifutayo:

KATIBU WA BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE,
S.L.P 686,
MPANDA-KATAVI.

IMETOLEWA NA,



TERESIA A. IRAFAY

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA (W) MLELE

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE.

Tarehe 20/10/2021

NAKALA

1. Mbao za Matangazo Halmashauri ya Wilaya ya Mlele
2. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mlele
3. Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa Katavi